

## **1.TANGAZO LA USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI (HOTEL LEVY)**

Kwa mujibu wa sheria ya nyumba za kulaza wageni ya mwaka 1972,kila Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anatakiwa kukata leseni ya biashara na kulipia ushuru wa nyumba ya kulala wageni kila mwezi.

Mmiliki anatakiwa kuwasilisha halmashauri kitabu cha wageni kwa ajili ya ukaguzi. Baada ya ukaguzi wa kitabu hicho, mmiliki hutakiwa kulipa asilimia 10% ya mapato yaliyopatikana katika mwezi husika.

Kwa mujibu wa sheria, ushuru huo hulipwa kuanzia tarehe 1 hadi 7 ya kila mwezi. Mmiliki anapochelewa kulipia katika tarehe hizo atatozwa adhabu ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja .

**TANGAZO LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA MANISPAA YA SONGEA.**

## **2.TANGAZO LA LESENI YA BIASHARA**

Kwa mujibu wa sheria namba 25 ya mwaka 1972 na sheria ya fedha namba mbili ya mwaka 2014 kila mtu au Taasisi inayotoa huduma au kuuza bidhaa,inatakiwa kukata leseni ya biashara ndani ya kipindi cha siku 21.

Kulingana na sheria hiyo,ni kosa kuendesha biashara au kutoa huduma bila kuwa na leseni ya biashara.mtu yeyote atakayebainika anaendesha biashara yake bila kuwa na leseni katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea atatozwa adhabu isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja.

Mfanyabiashara au mtoa huduma yeyote, unakumbushwa kukata leseni yako katika ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Songea kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

## **TANGAZO LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA MANISPAA YA SONGEA**

### **3.TANGAZO LA LESENI ZA VILEO**

Leseni za vileo hutolewa kwa mujibu wa sheria ya Leseni za vileo Na.28 ya Mwaka 1968 Leseni hizo hutolewa misimu miwili kwa mwaka yaani miezi sita sita.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea anawatangazia kuwa msimu wa kwanza wa leseni za vileo unaanza tarehe 1/10/ kila mwaka hadi tarehe 30/3/kila mwaka na kwamba msimu wa pili wa leseni za vileo unaanza tarehe 1/4/kila mwaka hadi 30/9/kila mwaka .

Kila mfanyabiashara anatangaziwa kuchukua fomu za maombi katika ofisi za Halmashauri ya manispaa ya songea kila msimu na kuirejesha fomu hiyo kabla ya mwisho wa msimu husika.

Mtu yeyote atakayebainika anaendesha biashara za vileo katika Bar,Grocery na Vileo, atatozwa adhabu isiyopungua shilingi laki mbili na isyozidi shilingi milioni moja.

**TANGAZO LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA MANISPAA YA SONGEA**